# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA KUMI NA TISA

**10 MEI, 2022**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 10 MEI, 2022

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**161. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo la Wagonjwa wa Nje, la X-Ray, la Watoto na Utawala katika Hospitali ya Wilaya Olturumet.

**162. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga nyumba za Walimu kama inavyofanya kwa Majeshi ya Ulinzi.

**163. MHESHIMIWA MWANTAKAJE HAJI JUMA (BUBUBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa mafunzo kwa makundi ya Vijana na Wanawake wanaopata mikopo ili waweze kujiwezesha kiuchumi.

**164. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaitengea bajeti barabara ya Kibaoni Kakunyu hadi Bugango Mpakani wakati taratibu za kupandishwa hadhi zikiendelea.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**165. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kushughulikia soko la ndani la Maziwa kwa kuhamasisha unywaji wa Maziwa shuleni.

**166. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED ABDALLAH (LINDI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo Kikuu cha Uvuvi na Usafirishaji Baharini katika eneo la Kikwetu ambapo tayari hekari 150 zimetengwa.

**WIZARA YA MAJI:**

**167. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Mradi wa maji wa Tukuyu utakamilika.

**168. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Kintinku - Lusilile katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**169. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha mifumo ya upatikanaji wa tiketi kwa wasafiri wa reli ya kati.

**170. MHESHIMIWA CONCHESTER LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja la Kalebe - Bukoba Vijijini ili kuwezesha magari yenye uzito zaidi ya tani kumi kupita kwenye Daraja hilo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**171. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya matukio ya moto katika masoko kwenye maeneo mbalimbali nchini.

## IV. KAULI ZA MAWAZIRI:

WAZIRI WA NISHATI:

## V. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**10 MEI, 2022**
**DODOMA**

**N.J. MWIHAMBI, ndc**
**KATIBU WA BUNGE**